# CHUMBA CHA UMOJA WA MATAIFA CHENYI KUWA NA DARAKA LA KUONGOZA MAMBO YA KIUTU – OCHA

# KANUNI ZA KUFUATA WAKATI WA UHAMISHO WA WATU NDANI YA INCHI YAO

**Utangulizi wa Katibu Mkuu Makamo, Bw.Sergio Vieira de Mello, kwa Kanuni za Kufuata wakati wa Uhamisho wa Watu Ndani ya Inchi yao**

Jamii ya Shirika za kiutu inaelewa shida za uhamisho zinazokumba zaidi ya watu milioni 20 katika dunia nzima. Ikiwa ulinzi wa watu waliohamishwa ndani ya inchi ni kazi ya Serikali za mataifa na ni mamlaka ya waongozi wa mahali kwanza, ni lazima jamii ya kimataifa ione namna gani inaweza kusaidia vizuri zaidi ukingo wa watu waliohamishwa ndani ya inchi katika hali za vita na shida. Ni lazima kwetu vilevile kufikiri juu ya musaada wa kiutu kwa namna inayoweza kuwezesha ukingo wa kutosha kwa watu waliohamishwa ndani ya inchi.

Katika matumikio ya Umoja wa Mataifa, mipango ya lazima sana imechukuliwa kwa kusaidia vizuri na vyepesi zaidi watu waliohamishwa ndani ya inchi katika mahitaji yao. Kamati ya kudumu kati ya Shirika za kimataifa imenipatia daraka la uteteaji katika kazi hii ya Umoja wa Mataifa kuhusu maswali yenyi kuelekea watu waliohamishwa ndani ya inchi. Kwa kutimiza kazi niliyopewa, nimeamua kutengeneza muzuri zaidi kazi ya Umoja wa Mataifa kwa kukabiliana na matatizo yanayotokana na uhamisho wa watu ndani ya inchi yao na kupendekeza

zaidi uongozi wa kipekee na ugawanyaji unaokuwa wazi zaidi wa madaraka ya kishirika; vilevile utoaji wa msaada unaotosha kwa Shirika tendaji.

Katika maoni haya, ninafurahi kujulisha watu wote kanuni za kufuata kwa ajili ya watu waliohamishwa ndani ya inchi (Watu waliohamishwa ndani ya inchi yao), kwa njia ya Mwakilishi wa kipekee wa Katibu Mkuu kwa watu waliohamishwa ndani ya inchi yao. Kanuni hizi zinazokuwa na msingi katika sheria ya kiutu ya mataifa, na vyombo vya kazi kuhusu haki za mwanadamu zinazofuatwa siku hizi, zitakuwa sawa kipimo cha mataifa kwa kuongoza serikali za inchi mbalimbali na shirika za kimataifa za kiutu na maendeleo kwa kutoa msaada na ukingo kwa watu waliohamishwa ndani ya inchi yao.

Kamati ya kudumu ya kimataifa inapokea vizuri sana kanuni za kufuata wakati wa uhamisho wa watu ndani ya inchi yao na iliwatia moyo wanamemba wake kwa kujulisha kanuni hizi kwa kundi zao za uongozi na wafanya kazi wao, hasa wale wanaokuwa mahali kazi zinafanyika, kusudi kanuni zitumiwe katika vitendo katika kazi wanazofanya kwa ajili ya watu waliohamishwa ndani ya inchi yao.

Ninaamini kwamba Kanuni hizi zinaweza kusaidia sana kwa kutambua mahitaji ya watu waliohamishwa ndani ya inchi yao. Kuamusha shirika za kiutu kuunga mkono na kusaidia watendaji wa kazi mahali watu waliohamishwa wanapokuwa kwa kutafuta na kutatua matatizo wanapoombwa kutatua mahitaji ya ukingo na usaidizi kwa waliohamishwa ndani ya inchi. Kanuni hizi zitasaidia serikali kutoa usalama na ustawi kwa watu waliohamishwa ndani ya inchi yao.

Ninatumaini kwamba kila mumoja wenu atajikaza kutawanya kanuni hizi na kuzitia kwa matendo vizuri kadiri inavyowezekana kwa kusudi la kufanya bora hali na uchukuaji wa watu wa waliohamishwa ndani ya inchi yao.

**Utangulizi wa Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Bw. Francis M. Deng, kuhusu Watu Waliohamishwa Ndani ya Inchi yao.**

Jamii ya kimataifa inakuwa na kazi kubwa ya kuhakikisha ukingo kwa watu waliongolewa kwa nguvu kutoka kwenye nyumba zao kutokana na mizozo au vita vikali, na kuzarau kwa hali ya juu haki za binadamu na mambo mengine ya kutisha, lakini watu hao wanabaki ndani ya nchi zao wenyewe. Karibu kwa mambo yote, hawa watu wananyimwa haki zao, wanateseka sana na wanabaguliwa. Ni kwa kupambana na matatizo haya ndipo kanuni hizi zimeandikwa.

Kanuni hizi zinafafanua haki na hakika zinazohusu ukikingo kwa watu waliohamishwa ndani ya inchi yao katika zote zyote za uhamisho. Zinatoa ukikingo juu ya uhamisho wa kiholela, shurti za ukingo na usaidizi wakati wa uhamisho, na hakika kwa kurudi, kupata makao mapya na kukutana tena na wajamaa katika usalama. Ingawa kanuni hizi si za kushurtisha, zinapatana na haki za binadamu za mataifa na sheria za ukimbizi.

Kwa hiyo, mambo ya muhimu kufuatana na kazi niliyotolewa ilikuwa ni kuweka utarabitibu wa kikanuni na njia za kufuata kisheria kwa ajili ya wakimbizi na kupanga safari katika inchi mbalimbali kwa kusudi ya kuweka uwezekano wa mazungumuzo pamoja na serikali na wateteaji wengine wa haki za wakimbizi. Pamoja na kundi la wataalamu wa kisheria wa kimataifa, nilijifunza kiasi gani haki ya watu waliohamishwa ndani ya inchi yao inachukuliwa ndani ya sheria za kimataifa. Basi niliweka pamoja maandishi ya kisheria na niliweka uchunguzi wa kanuni za kisheria (E/CN.4/1996/52/Add.2) uchunguzi uligundua kwamba ilhali sheria iliyoko sasa ina toa taarifa za matukio thabiti kwa waliohamishwa kindani, kuna eneo kuu ambamo inashidwa kutoa msingi imara kwa kinga yao na usaidizi. Kisha, Tume na mkutano wa wote viliniomba kutayarisha mfumo sanifu unaofaa kwa waliohamishwa kindani. Hili lilisababisha

uandikaji mswada wa kanuni ongozi ambazo zinataja tena kaida zilizoko na zinaomba ubainishaji wa eneo zisizo dhahiri na kujaza mapengo.

Baada ya kutoa kanuni ongozi kwa Tume katika 1998, Tume ilikubali azimio ikitambua kanuni ongozi na kusudi langu lililotajwa kama mwakilishi wa Katibu mkuu kuzitumia katika maongezi yangu yanayoendelea na serikali na hao wote ambao udhamini wao na vitendo vinahusiana na mahitaji ya waliohamishwa kindani. Tume pia ilitambua uamuzi wa Kamati inayosimama kati ya mawakala ambayo ilikuwa imekaribisha kanuni na kutia moyo wanajumuiya wake kuzigawana na bodi za utendaji zao na wafanyakazi, hasa uwanjani, na kuzitumia katika vitendo vyao kwa niaba ya waliohamishwa kindani.

Kanuni ongozi zapaswa kutoa uongozi wa thamani wa utendi kwa serikali, wenye mamlaka hodari, vyama vilivyo kati ya serikali na vyama visivyo vya serikali “NGOs” katika kazi zao na watu waliohamishwa kindani. Ni tumaini langu kwamba zitaenea kwa mapana na kupewa matumizi ya utendi uwanjani.

**Kanuni za kufuata kwa uhamisho wa ndani**

(1) Kanuni hizi zinalenga kusaidia mahitaji ya kipekee ya watu waliohamishwa ndani ya inchi yao katika dunia nzima. Hizi kanuni zinatambulisha haki na hakika kuhusu ukingo wa watu waliohamishwa kwa kinguvu na kuwakinga na kuwasaidia wakati wa uhamisho wao na wakati wa kurudi kwao au wakati wa kupata makao mapya na kuwastarehesha tena.

(2) Kwa makusudi ya kanuni hizi, watu waliohamishwa ndani ya inchi yao, ni watu au vikundi vya watu ambao wamelazimishwa au wamesukumwa kuacha au kukimbia nyumba zao au makao yao, kufuatana na vita au kufuatana na mizozo ya kivita, au

mazarau ya haki za binadamu au kufuatana na vurugu za kimaumbile au vurugu zilizosababishwa na binadamu au kwa sababu ya kuepuka matokeo ya vurugu hizo, na ambao hawakuvuka mipaka ya inchi inayotambulikana kimataifa.

(3) Kanuni hizi zinaonyesha sheria ya kimataifa inayohusu haki za binadamu na haki ya kimataifa ya kiutu na zinakubaliana na sheria hiyo ya kimataifa. Zinakusudia kuongoza :

a. Mwakilishi wa Katibu mkuu anayehusika na watu waliohamishwa ndani ya inchi yao kwa muda wa kazi yake ;
b. Mataifa yanapokabiliana na mambo ya uhamisho wa watu ndani ya inchi yao;
c. Makundi mengine ya watu, wakubwa au watu wanahusika na WATU WALIOHAMISHWA NDANI YA INCHI YAO WENYEWE ; na
d. Shirika au Vyama vya serikali na vile visivyo vya serikali vinaposhughulikia uhamisho wa ndani

**(4)** Kanuni hizi zinapaswa kutangazwa kwa enezi na kutumiwa sana kadiri iwezekanavyo.

**Sehemu ya I: Kanuni za jumla**

**Kanuni ya I**

1. Watu waliohamishwa ndani ya inchi yao wanakuwa na haki na uhuru sawasawa na wanainchi wenzao mbele ya sheria ya kimataifa na mbele ya sheria ya inchi yao. Hawatabaguliwa katika kuhusu utimizaji wa haki na uhuru wowote kulingana na hali yao kama watu waliohamishwa ndani ya inchi yao.
2. Kanuni hizi hazionyeshe hata kidogo kwamba watu waliohamishwa ndani ya inchi yao ni washitakiwa wa sheria ya kimataifa, hasa kuhusu mauaji ya kuangamiza (génocide), au kuhusu kosa juu ya kiutu na kosa juu ya kanuni za vita.

**Kanuni ya 2**

1. Bila kuhusika na utambulisho kisheria, Makundi ya watu, wakubwa au watu wote wanapaswa kutimiza kanuni hizi pasipo ubaguzi wa aina yoyote. Utimizaji wa kanuni hizi hauhusike kisheria na hali ya wakubwa, makundi au watu wanaohusika.
2. Kanuni hizi haizipaswi kuonekana kama vile zinapunguza, kugeuza au zinazaifusha haki za binadamu za kimataifa zote, au vifaa vya sheria ya kimatifa ya kiutu au haki zilizopewa watu chini ya sheria za inchi. Kwa upekee, kanuni hizi hazina shida kwa haki ya kutaka na kupata makimbilio katika nchi nyingine.

**Kanuni ya 3**

1. Wakubwa wa kimataifa wanahusika wa kwanza na shurti ya kutolea watu waliohamishwa ndani ya inchi yao ukingo na usaidizi katika eneo ya mamlaka yao.
2. Watu waliohamishwa ndani ya inchi yao wanakuwa na haki ya kuomba na kupokea ukingo na usaidizi wa kiutu kutoka wakubwa hawa. Hawapaswi kuona mateso ya aina yoyote au kuazibiwa kwa kufanya ombi la aina hiyo.

**Kanuni 4**

1. Kanuni hizi zitatumiwa bila ubaguzi wa aina yoyote, kama: rangi, kimaumbile, luga, dini au imani, siasa au msimamo mwingine, taifa au kabila au aina yoyote ya ukabila, sheria au kazi ya kijamii, utambulisho kisheria au kijamii, ulemavu, uenyeji wa kitu, kuzaliwa au shurti nyingine zozote za utambulisho wa mtu kama hizi.

2. Watu wengine kati ya waliohamishwa ndani ya inchi yao, kama vile watoto, hasa watoto wasiosindikizwa, wanawake wenye mimba, wamama wenye kuwa na watoto wadogo, viongozi vya kike vya familia, watu wenye ulema, na wazee, watapewa haki ya ukingo na usaidizi unaohitajika kwa hali yao na kwa kushugulikiwa kulingana na mahitaji yao ya kipekee.

**Sehemu ya II. Kanuni zinazohusu ukingo juu ya Uhamisho**

**Kanuni ya 5**

Wakubwa wote na watu wote wenye kuhusika kimataifa wataheshimu shurti zinazowaelekea kufuatana na sheria ya kimataifa, hasa haki za binadamu na sheria ya kiutu, katika hali zote, kwa kusudi la kukinga na kuzuia hali zinazoweza kuleta uhamisho wa watu.

**Kanuni ya 6**

1. Kila mutu anakuwa na haki ya kukingwa juu ya kuhamishwa ovyo kutoka kwa nyumba yake, kwa makao au kwa mahali yake ya kuishi.
2. Katazo kwa uhamisho wa ovyo linakuwa :
   (a) kwa uhamisho unaokuwa na msingi juu ya hali za ubaguzi: unaojulikana kama "usafishaji wa kikabila", yaani uaji wa kikabila, au vitendo kama hivyo vinavyolenga ugeuzaji wa kabila, wa dini au wa rangi kwa watu wanaohusika;
   (b) kwa uhamisho unaotokana na hali za mizozo ya kivita, isipokuwa usalama wa watu wanaohusika au kwa sababu za kijeshi zinazohitajika;

(c) kwa uhamisho unaofuatana na miradi mikubwa ya maendeleo, ambayo hayakubaliwe na watu wote kifaida;

(d) kwa uhamisho ambao unafanyika kutokana na hatari ya mahali, isipokuwa usalama na afya ya wale wanaohatarika vinahitaji uhamishaji na

(e) kwa uhamisho unaotumiwa kama njia ya kuazibu watu wote kwa mara moja.

3. Uhamisho hautaendelea kuzidi hali ya mambo inavyotaka.

**Kanuni ya 7**

1. Mbele ya kuamua watu wahamishwe, wakubwa wanaohusika wajaribu kuchunguza njia nyingine kwa kuepuka kuchukua uamuzi wa namna hii ya uhamisho kwa jumla. Kama hakuna namna ingine ya kufanya, wakubwa wajikaze kupunguza idadi ya watu kwa uhamisho na hatari zake mbaya.
2. Wenye mamlaka wanaoendesha uhamisho kama huo, watajikaza kwa namna yote watu wapangishwe vizuri, kazi ifanyike vizuri kwa mambo yenye kuangalia usalama, malisho, afia na usafi, na kwa ginsi watu wa jamaa moja wasitenganishwe.
3. Wakati uhamisho unatokea katika hali nyingine zisizokuwa za haraka kutokana na mizozo ya kivita ao hali ingine ile ya hatari, inapaswa kuhakikishwa mambo haya:

(a) Wakubwa wenye mamlaka kutokana na sheria ndio wanakuwa na haki ya kuamuru hatua za uhamisho wa watu;

(b) Inafaa kufanya mpango mzuri kusudi watu wanaohamishwa ndani ya inchi yao wajulishwe waziwazi visababu vya uhamishaji na taratibu zitakazofuatwa kwa uhamisho wao na kama inahitajika, kuwajulisha haki au makao yao mapya.

(c) Inafaa kupata ukubali kwa hiari na unaojulikana kwa wale watakaohamishwa.

(d) Wenye mamlaka wanaohusika watajitahidi kushughulisha wale wanaokuwa katika hali ya hatari hasa wanawake, katika upangaji na uongozi wa makao mapya yao.

(e) Hatua za kulinda utaratibu pale zinapohitajika, zitachukuliwa na wenye mamlaka kisheria wanaofaa;

(f) Zitaheshimiwa vilevile haki kwa kutafuta usaidizi unaofaa, mukiwa kuchunguza upya uamuzi kama huo na wakubwa wa kisheria wanayofaa.

**Kanuni ya 8**

Uhamisho hautafanywa katika njia zinazozarau haki kwa kuishi, kwa heshima, kwa uhuru na usalama wa wale wanaokuwa katika hatari.

**Kanuni ya 9**

Mataifa yanashurtishwa kwa upekee kukinga watu wa asili, watu wanakuwa kwa uchache, watu wanaokaa katika vijiji, wafugaji wa nyama na vikundi vingine wanaotegemea na kushikilia mahali ya makao yao.

**Sehemu ya III. Kanuni zinazohusu ulinzi wakati uhamisho unatendeka**

**Kanuni ya 10**

1. Kila mwanadamu ana haki inayofungwa na maisha ambayo yatalindwa na sheria. Hakuna mtu atakayenyimwa maisha yake ovyo. Watu waliohamishwa ndani ya inchi yao watalindwa kwa upekee juu ya:

    (a) Mauaji ya kuangamiza

(b) Mauaji ya mtu kwa mtu

(c) Mauaji ya kiserikali ovyo ovyo; na

(d) Kukaza watu kupotea, kama vile kuwakamata mateka au kuwafunga pasipo julikana, kwa kuwatisha au kwa kuwaua.

Kufanya vitisho vya namna hii na kuchochea mambo haya yote, ni vitendo vinavyokatazwa.

2. Mashambulio au vitendo vingine vya mgogoro juu ya watu waliohamishwa ndani ya inchi yao ambao hawashiriki tena katika mizozo au migogoro ya vita vimekatazwa kwa hali yoyote. Watu waliohamishwa ndani ya inchi yao watakingwa kwa upekee juu ya:
   (a) Mashambulizi waziwazi ao mashambulizi yasiyotofautisha au vitendo vingine vya mgogoro, kama vile kusema maneno ambamo mashambulizi kwa raia yanaruhusiwa.
   (b) Kunyima chakula kama njia ya mapambano
   (c) Kutumia watu waliohamishwa ndani ya inchi yao kama ukingo wa nia za kijeshi juu ya ushambulizi au kwa kukinga, kupendelea au kuzuiza utendaji wa jeshi.
   (d) Mashambulizi juu ya kambi au maeneo ya makao yao ; na
   (e) Matumizi ya mabomu ya chini kwa chini za kuua watu.

**Kanuni ya 11**

1. Kila mutu ana haki kwa heshima na ukamilifu wa mwili, akili na tabia.
2. Watu waliohamisha ndani ya inchi yao, iwe uhuru wao umezuiliwa au hapana, watalindwa kwa juu ya :

(a) Kubakwa au kufanya mapenzi kwa kingufu, kukata sehemu za mwili, kutesa, kutendea mutu vibaya sana, kwa njia isiyo ya kiutu au kwa njia inayopunguza heshima au adabu na vitendo viovu vingine juu ya uhuru wa mtu, kama vitendo vya migogoro inayovizia wanawake, kama vile ukahaba wa kinguvu, na mtindo wowote wa mashambulio ya kupatisha mtu haya wazi wazi;

(b) Utumwa au mtindo wowote wa kisasa wa utumwa, kama vile ununuzi wa watu kwa shabaa za ndoa, kutumia mamlaka kwa kufanya kitendo cha ndoa au kazi ya kimakazo kwa watoto; na

(c) Vitendo vya ukali sana vinavyokuwa na shabaa ya kueneza woga kati ya watu waliohamishwa ndani ya inchi yao.

Vitisho na uchocheaji wa kutenda mambo haya yote vitakatazwa.

**Kanuni ya 12**

1. Kila mwanadamu ana haki kwa uhuru na Usalama wa mtu. Hakuna mtu atakayekamatwa ao kufungwa ovyo.
2. Kutia uzito kwa haki hii kwa watu waliohamishwa ndani ya inchi yao, hawatafungwa au kuwekewa mipaka katika kambi. Ikiwa katika hali za kipekee, kufunga ao kuweka mipaka ni kwa lazima, mipango hii haitaendelea kudumu kuliko inavyohitajika.
3. Watu waliohamishwa ndani ya inchi yao watalindwa juu ya kukamatwa na kufungwa kama jambo hilo linatokea kwa hali ya uhamisho wao.
4. Hakuna hali yoyote ambamo watu waliohamishwa ndani ya inchi yao watakamatwa mateka.

**Kanuni ya 13**

1. Hakuna hali yoyote ambamo watoto waliohamishwa wataingizwa katika jeshi lolote ao kukazwa ao kuruhusiwa kushiriki mambo ya kivita.
2. Watu waliohamishwa ndani ya inchi yao watalindwa juu ya mazoezi yanayobagua ambayo yanatoa faida kutoka hali yao kwa kuwaingiza katika vikosi vyenye silaha ao vikundi vyenye silaha. Kwa upekee, matendo yoyote ya uuaji, mazoezi ya kinyama au yanayoshusha heshima ya kiutu ambayo yanashurutisha mtu aliye katika uhamisho kukubali kuingia katika kikundi cha kijeshi ao kwa kuazibu wasiokubali kwa kujiandikisha vinakatazwa katika hali yoyote.

**Kanuni ya 14**

1. Kila mtu aliyehamishwa ndani ya inchi yake ana haki ya uhuru wa kuhama na uhuru wa kuchagua makao yake.
2. Kwa upekee, watu waliohamishwa wana haki ya kuhama kwa uhuru ndani na inje ya kambi ao makao mapya katika mahali popote ambapo maisha, usalama , uhuru, na/ao afya yao ingekuwa kwa hatari.

**Kanuni ya 16**

1. Watu wote aliohamishwa ndani ya inchi yao wanakuwa na haki ya kujua kilichowafikia ao mahali watu wa jamaa yao wanakuwa.
2. Wakubwa wanaohusika watajikaza kutambua kilichowafikia watu waliohamishwa ndani yao na mahali watu wao wanapokuwa, yaani watu ambao wameripotiwa kuwa

wamekosekana; na watashirikiana na vyama vya kimataifa vinavyoshughulikia kazi hii. Watawajulisha ndugu wao wa karibu juu ya maendeleo ya uchunguzi na kuwajulisha matokeo yoyote.

3. Wakubwa wanaohusika watajikaza kukusanya, na kutambua mabaki ya miili ya marehemu, watazuia maiti yasioze na yasishikwe vibaya, na watarudisha mabaki hayo kwa ndugu wa karibu ao kuyazika kwa heshima.
4. Kaburi za watu waliohamishwa ndani ya inchi yao zinalazimika kulindwa na kuheshimiwa kwa hali yoyote. Watu waliohamishwa ndani ya inchi yao wanapaswa kuwa na haki ya kufika kwenye kaburi ya marehemu waliokuwa wajamaa wao.

**Kanuni ya 17**

1. Kila mwanadamu anakuwa na haki ya heshima kwa jamaa yake.
2. Kutia uzito kwa haki hii kwa watu waliohamishwa ndani ya inchi yao, wanamemba wa jamaa ambao wanapenda kubaki pamoja, watakubaliwa kufanya hivyo.
3. Jamaa ambazo zimetenganishwa sababu ya uhamisho ziunganishwe tena haraka inavyowezekana. Hatua zote zinazofaa zitachulikuwa kwa kuharikisha uunganaji tena wa jamaa kama hizo, hasahasa, kama watoto wamehusika. Wakubwa wanaohusika, watarahisisha maulizo yanayofanywa na wanamemba wa jamaa na kuwatia moyo na kushirikiana na kazi ya vyama vya kiutu vinavyoshughulikia kazi ya kuunganisha jamaa tena.
4. Wanamemba wa jamaa zilizohamishwa ndani ya inchi yao ambao uhuru umezuiliwa na kufungwa ao kuwekewa mipaka katika kambi watakuwa na haki ya kubaki pamoja.

**Kanuni ya 18**

1. Watu wote waliohamishwa ndani ya inchi yao wanakuwa na haki kwa kiwango kinachofaa kwa kuishi.
2. Kiwango hicho kikiwa kidogo, bila kujali hali na bila kubagua, wakubwa wenye kuhusika watawapa watu waliohamishwa ndani yao usaidizi ufuatao na watahakikisha kwamba usaidizi huu utawafikia salama:
   (a) Chakula kinachohitajika na maji ya kukunywa
   (b) Mahali ya kupumzikia kwa muda na nyumba
   (c) Mavazi yanayofaa; na
   (d) Matunzo ya afya yanayohitajika na usafi wa mazingira.
3. Inafaa ihakikishwe sana kwamba wanawake wanashirikishwa kikamilifu katika mipango na ugawanyaji wa misaada ya msingi.

**Kanuni ya 19**

1. Watu waliohamishwa ndani ya inchi yao wenye kuwa na majeraha au wagonjwa pamoja na wale wenye ulema watapokea kadiri inavyowezekana na bila kukawia matunzo na musaada wanaohitaji, bila ubaguzi unaokuwa na visababu vyovyote isipokuwa matunzo. Ikihitajika, watu waliohamishwa ndani ya inchi yao watawezeshwa kufika kwa misaada za kisaikolojia na za kijamii.
2. Uangalifu wakipekee utawekwa kwa mahitaji ya kiafya ya wanawake, kama vile kufika kwa waganga na watunzaji wa afya wa kike na kazi, kama vile kutunza afya ya uzazi pamoja na mashauri yanayofaa kwa waliokuwa mateka wa ngono na matusi mengine.

3. Uangalifu wakipekee vilevile utapewa kwa kuzuiza magonjwa ya kuambukiza na ya enezi, kama vile UKIMWI katikati ya watu waliohamishwa ndani ya inchi

**Kanuni ya 20**

1. Kila mwanadamu anakuwa na haki ya kutambuliwa popote kama mtu mbele ya sheria.
2. Kutia uzito kwa haki hii kwa ajili ya watu waliohamishwa ndani ya inchi yao, wakubwa wanaohusika watawapa vyeti vyote vya utambulisho vinavyohitajika kwa kuwawezesha kupata faida ya haki zao inavyofaa, kama vile: pasipoti, vyeti vya kuzaliwa na vyeti vya ndoa. Kwa upekee, wenye mamlaka watarahisisha jambo la kuwapa vyeti vipya au kuviweka tena vile vilivyopotea wakati wa uhamisho, bila kuweka masharti yasiyo ya maana, kama vile, kuhitajika kurudi kwa eneo la makao ya kawaida, ili kupata hivi au vyeti vingine.
3. Wanawake na wanaume watakuwa na haki sawa kupata vyeti kama hivi vinavyohitajika na watakuwa na haki ya kupata vyeti kama hivi katika majina yao wenyewe.

**Kanuni ya 21**

1. Hakuna mtu atakayenyimwa vitu na mali yake ovyo.
2. Vitu na mali ya watu waliohamishwa ndani ya inchi yao vitalindwa kwa hali yoyote, kwa upekee juu ya vitendo vifuatavyo.
   (a) Uporaji
   (b) Mashambulizi ya moja kwa moja au yasiyotofautisha au vitendo vingine vya mgogoro.
   (c) Kutumiwa kama ukingo kwa vitendo ao malengo ya kijeshi

(d) Kutumiwa kama chombo cha kulipiza kisasi; na

(e) Kuharibiwa au kuchukuliwa kama aina ya azabu ya jumla.

3. Vitu na mali vilivyoachwa nyuma na watu waliohamishwa vitalindwa kusudi visiharibike na kuchukuliwa, kutumiwa au kuvikamata ovyo.

**Kanuni ya 22**

1. Watu waliohamishwa ndani ya inchi yao wanaoishi katika kambi ao nafasi ingine, hawatabaguliwa kwa sababu ya hali ya uhamisho kwa kupata faida ya haki zao zifuatazo:

   (a) Haki za uhuru wa kufikiri, zamiri, dini au musimamo, mawazo na kujieleza

   (b) Haki ya kutafuta kwa uhuru nafasi za kazi na kushughulika na vitendo vya kiuchumi

   (c) Haki ya kuungana na watu kwa uhuru na kushiriki kwa usawa katika mambo ya jamii.

   (d) Haki ya kupiga kura na kushirikishwa katika mambo ya kiserikali na ya raia; kama vile haki yakufika njia zinazohitajika kutenda haki hii; na

   (e) Haki ya kuwasiliana katika Luga wanayofahamu.

**Kanuni ya 23**

1. Kila mwanadamu ana haki kwa Elimu;
2. Kutia uzito kwa haki hii kwa watu waliohamishwa ndani ya inchi yao, wakubwa wanaohusika watahakikisha kwamba watu kama hao, kwa upekee watoto

waliohamishwa, wapokee Elimu itakayokuwa huru na ya lazima kwa kiwango cha msingi. Elimu inapaswa kuheshimu utambuzi wao wa kitamaduni, luga na dini;

3. Inafaa kuhakikisha kwamba wanawake na wasichana wanashirikishwa vizuri na kwa usawa katika taratibu za Elimu.
4. Elimu na vifaa vya masomo vitatolewa kwa watu waliohamishwa ndani ya inchi yao, wakati itakavyowezekana, hasa kwa vijana na wanawake wakiishi katika kambi ao sivyo.

**Sehemu ya IV. Kanuni zinazohusiana na usaidizi wa kiutu**

**Kanuni ya 24**

1. Usaidizi wote wa kiutu utatolewa kulingana na kanuni za kiutu bila upendeleo na ubaguzi.
2. Msaada wa kiutu kwa watu waliohamishwa ndani ya inchi yao hautatumiwa kwa kazi ingine, hasa kwa sababu za siasa au za kijeshi.

**Kanuni ya 25**

1. Daraka la msingi na wajibu wa kutoa msaada wa kiutu kwa watu waliohamishwa ndani ya inchi yao viko katika mikono ya wenye mamlaka ya kitaifa.
2. Vyama vya kiutu vya kimataifa na Watenda kazi wengine wanaofaa, wana haki ya kutoa kazi zao kuunga mkono watu waliohamishwa ndani ya inchi yao. Musaada kama huu hautaangaliwa kama kitendo kisicho cha urafiki au kiingilio katika mambo ya ndani ya taifa, na kitafikiriwa kwa moyo mwema. Ukubalifu kwa vyama hivyo hautazuiliwa ovyo, kwa upekee wenye mamlaka wanaohusika wasipoweza au wasipotaka kutoa msaada wa kiutu unaohitajika.

3. Wenye mamlaka wote wanaohusika watajalia na kurahisisha mambo kusudi msaada wa kiutu upite kwa uhuru na kuwajilia watu wanaoshughulika katika utoaji wa msaada kama huo ili ufike kwa haraka na usiozuiliwe, kwa watu waliohamishwa ndani ya inchi yao.

**Kanuni ya 26**

Watu wanaoshughulika katika msaada wa kiutu, usafirishaji wao na vifaa vyao vitaheshimiwa na kulindwa.  Hawapaswi kushambuliwa au kufanyiwa vitendo vingine vya mgogoro.

**Kanuni ya 27**

1. Vyama vya kimataifa vya kiutu na watenda kazi wengine wanaofaa, wanapotoa msaada, wanapaswa kuangalia mahitaji ya ulinzi na maisha za binadamu vya watu waliohamishwa ndani ya inchi yao na kuchukua hatua zinazofaa kuhusu jambo hili.  Kwa kufanya hivi, vyama hivi na watendi kazi vinapaswa kuheshimu viwango vya kimataifa vinavyohusika na kanuni za mwenendo mema.
2. Yanayosemeka hapa juu hayamaanishe lo lote kuhusu wajibu kwa mambo ya ulinzi wa vyama vya kimataifa vilivyotumwa kwa nia hii, ambavyo kazi zake zitapewa au kuombwa na mataifa.

**Sehemu ya V: Kanuni zinazohusu kurudi, kupata makao mapya na kukusanyika tena.**

**Kanuni ya 28**

1. Wenye mamlaka wanaofaa wana daraka ya msingi na wajibu kuweka masharti pamoja na kutoa njia zinazoruhusu watu waliohamishwa ndani ya inchi yao kurudi kwa hiari yao katika usalama na heshima, kwa nyumba zao au makao yao, au kupata makayo mapya

kwa hiari yao katika sehemu nyingine za nchi.  Wakubwa kama hao watajilazimisha kurahisisha ustarehe wa watu waliorudi au kupata wakao mapya, ambao walikuwa wamehamishwa ndani ya inchi.

2. Inafaa kabisa kuhakikisha kwamba watu waliohamishwa ndani ya inchi yao wanashirikishwa vizuri katika mpango na uongozi wa kurudi kwao na kukusanyika tena…

**Kanuni ya 29**

1. Watu waliohamishwa ndani ya inchi yao ambao wamerudi kwa nyumba zao ao kwa makao yao au ambao wamepata makao mapya katika sehemu nyingine za inchi, hawatabaguliwa kwa sababu ya hali ya uhamisho.  Watakuwa na haki kushiriki vikamilifu na kwa usawa katika mambo ya umma kwa kiwango chochote na kufika sawa kwa kazi za umma.
2. Wenye mamlaka wanaofaa wana kazi na wajibu ya kuwasaidia waliorudi na/au waliopata makao mapya ambao walikuwa wamehamishwa ndani ya inchi, kupata tena, kwa kiasi kinachowezekana, mali yao na vitu ambavyo waliacha nyuma au walipohamishwa. Kupata tena mali na vitu kama hivyo isipowezekana, wenye mamlaka wanaofaa  watatoa au watasaidia watu hawa kupata malipo yanayofaa au mtindo mwingine wa kupewa tena vitu walivyopoteza.

**Kanuni ya 30**

Wenye mamlaka wote wanaohusika wataruhusu na kusaidia vyama vya kimataifa vya kiutu na vyama vingine vingine vinavyofaa kufikia, katika utimizaji wa kazi zao,  kwa haraka na

bila shida watu waliohamishwa ndani ya inchi kwa kuwasaidia kurudia ao kustarehe katika makao yao mapya ao kujikusanya tena.